**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA UKEREWE**

**MTIHANI WA KIDATO CHA TATU**
**021 KISWAHILI**

**Muda : Saa 3:00** **Mwaka: 2025**

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, na C zenye jumla ya maswali kumi na moja (11).
2. Jibu maswali yote katika sehemu A na B na maswali mawili tu kutoka sehemu C.
3. Sehemu **A** ina alama **16,** sehemu **B** alama **54** na shemu **C** ina alama **30**

## **SEHEMU : A** (alama 16)

Chagua jibu sahihi katika kipengele (i) – (x) Kisha andika jibu sahihi katika karatasi za kujibia

i "Mimi ni ncha ya mkuki sipigwi kozi wala sipigwi kwa chochote jaribu utakiona cha mtemakuni nilishinda pia vita katika vita ya kagera na Uganda" Je ni aina gani ya Kipera katika fasihi kati ya hivi vifuatavyo:-

A. Ngomezi
B. Ushairi
C. Majigambo
D. Ngonjera
E. Methali

ii. Mwajuma alipopewa maswali na Mwalimu wake wa Kiswahili akayajibu kwa haraka lakini ndani ya majibu yale moja lilikuwa sahihi zaidi, ni lipi kati ya haya yafuatayo kuhusu kamusi.

A. Fani na maudhui
B. Tahakiki za wanafasihi
C. Muktadha wa matumizi ya kamusi
D. Mfano wa michoro ya samaki, wanyama na wadudu

iii. Marejeo ya orodha ya maneno yaliyopangwa kwa utaratibu maalumu unaofuata alfabeti Jirani alipoambiwa ataje watoto mapacha waliokuwa wakiishi kwenye familia ya mzee John Walirandana na kutofautiana . Taja jozi yenye kufanana na mapacha hao kitanzu katika fasihi.

A. Vitenzi, kamusi, viunganishi na hadithi
B. Hadithi, ushairi, maigizo na semi
C. Ushairi, mashairi, maigizo na semi
D. Maigizo, semi ngonjera na semi
E. Semi, maigizo, nudhumu na mapingiti

iv. Ili kukamilisha mawasiliano miongoni mwa watumiaji lazima kuzingatia vitamkwa ambavyo ni msingi katika lugha ya Kiswahili. Miongoni mwa vitamkwa hivyo ni:-

A. Irabu na konsonanti
B. Silabi na irabu
C. Konsonanti na neno
D. Sauti na silabi
E. Neno na neno

v. Mama <u>na</u> bibi wamekwenda sokoni kununua mchele. Je, ni aina gani ya kiunganishi ilivyotumika kati ya hivi vifuatavyo

A. Kiunganishi husishi
B. Kiunganishi huru
C. Kiunganishi tegemezi

D. Kiunganishi cha a – unganifu
E. Kiunganishi kiwezeshi.

vi. Miongoni mwa malengo ya ufupishaji habari, huwa ni kwasababu ya :-
A. Ukweli wa mambo yanayozungumzwa
B. Kuandika habari kwa kutumia mawazo maku kutoka kwenye habari iliyosimuliwa.
C. Kujua ukweli wa mambo yanayozungumzwa katika jamii
D. Ili kusoma vitabu vya hadithi mbalimbali kila siku
E. Kujua kusoma na kuandika habari

vii. Mama ameletewa zawadi ya sukari kwaajili ya kumbukumbu ya kuzaliwa kwake. Je, neno sukari limetumia ngeli ya :-
A. A –WA
B. U – I
C. LI – YA
D. KI – VI
E. I – I

viii. Mwalimu alimwambia mthibiti ubora kuwa “ kipindi kimeanza” Mwalimu alitumia aina gani ya tungo kati ya tungo zifuatazo?
A. Tungo neno
B. Tungo kirai
C. Tungo kishazi
D. Tungo sahihi
E. Tungo sentensi

ix. “Nyumba imeezekwa lakini inavuja sana” sentensi hii iliongelewa / zungumzwa na baba mwenye nyumba hiyo. Je alitumia aina gani ya sentensi ili kutoa ujumbe?
A. Sentensi ambatano
B. Sentensi changamano
C. Sentensi shurutia
D. Sentensi sahili
E. Sentensi ya tungo

x. Kazi iliyoandaliwa na kusomwa na mkuu wa wilaya siku ya Nyerere tarehe 14/10/2023 ilitumia mambo mawili katika kuhakikiwa ambayo ni:-
A. Muundo na mtindo
B. Mtazamo na msimamo
C. Wahusika na Mandhari
D. Fani na maudhui
E. Ujumbe na dhamira

2. Oanisha maneno yaliyopo katika orodha “A” nay ale ya orodha “B” ili yalete maana.

| ORODHA ‘A’ | ORODHA ‘B’ |
|---|---|

| | |
|---|---|
| I. Vichekesho<br>II. Riwaya fupi<br>III. Mkondo wa kiwasifu<br>IV. Ramsa<br>V. Riwaya thati<br>VI. Mkondo wa kihistoria | A. Masuala ya imani za kishirikina<br>B. Zawadi ya ushindi (1992)<br>C. Hutekenya hisia za watazamaji na kuwafanya waangue kicheko<br>D. Visa vichache<br>E. Nimfano wa riwaya ya barua ndefu kama hii<br>F. Visa vyake hujikita katika maisha na uwepo wa kifo<br>G. Riwaya ya maisha yangu baada ya miaka hamsini (2003)<br>H. Riwaya ya hiba ya wivu(1997)<br>I. Vita ya Idd Amin Dadah wa Uganda dhidi ya Tanzania |

**SEHEMU "B"** (alama 54)

Jibu maswali yote katika sehemu hii

3. a) Eleza dhima za mofimu **"li"** kama ilivyotumika katika sentensi zifuaatazo:-
   i. Shamba letu **l**i kubwa sana.
   ii. Wa**li**chelewa kurudi.
   iii. Tuna**li**fuatilia
   iv. **Li**meharibika
   v. Shiki**li**a

b) Kwa kutumia uelewa ulioupata katika somo la Kiswahili, ainisha sentensi (i) – (iv) kisha bainisha muundo wa kila sentensi.
   i. Ugonjwa wa Ukimwi hautibiki wala hauna kinga
   ii. Shule zote zilifungwa ulipoingia ugonjwa wa mlipuko
   iii. Ajali haina kinga
   iv. Ungenisalimia ningekuitikia.

4. **(**a) Ukiwa kama mtaalamu wa lugha ya Kiswahili bainisha makosa matano ya kisarufi yanayofanywa na watumiaji wa lugha ya kiswahili.
   (b) kwa kifupi eleza mambo manne yanayounda lugha kifasihi.

5. Kumbukumbu za maandishi husaidia kutunza historia za watu au vitu mbalimbali ambayo husaidia katika kurejelea ukweli wa mambo hasa kunapoibuka ubishani. Kubaliana na kauli hii kwa hoja sita huku ukirejelea asili ya kiswahili.

6. Kuna kundi la wanafunzi wanaojifunza Kiswahili nchini ughaibuni wamekuja Tanzania kufanya utafiti wa lahaja za Kiswahili. Wewe ukiwa ni mwenyeji wao na ni mbobezi wa lugha ya kiswahili wasaidie kujua lahaja sita za Kiswahili na sehemu zinapozungumzwa.

7. Lugha ina tabia ya kujiongezea msamiati wake kwa njia kadha wa kadha..kwa kuthibitisha dai hilo, tambulisha.njia zilizotumika kuunda maneno yafuatayo.

i.Kuku ii.Mpangaji iii.Kifaurongo iv.TATAKI v.Fedha vi.Msikwao vii.Kitivo viii.Pilipili ix.Imla,Mali,Mila,Lami

8. Kwa kutumia tamthilia ya "NGOSWE PENZI KITOVU CHA UZEMBE" na "KILIO CHETU" .Eleza kwa ufupi mambo matatu kwa kila mmoja yanayomfanya Ngoswe na Mama Suzi kulaumiwa na jamii.

**SEHEMU "C" ( alama 30)**

**Jibu maswali mawili (2) tu katika sehemu hii swali la 09 ni lazima**

9. Methali ni semi za busara ambazo hutoa maonyo mbali mbali katika jamii. Kwa kutumia methali sita (6) unazozifahamu eleza ni kwa namna gani hutoa maonyo mbali mbali kwa jamii.

10. Wenye utu husema, "Mtoto wa mwenzio ni mwanao." Lakini Wasio nao husema, "Pilipili i shambani, mjini ikuwashie nini?" Kwa kumtumia B.J Hanson na E. Mbogo Au E. Mbogo na A.J Safari, Au A.J Safari na B.J Hanson dhihirisha usawiri wa.kauli ya wasio na utu katika jamii.Tumia hoja sita.

11. "Uchaguzi wa majina ya vitabu husaidia kuibua dhamira za mwandishi" Thibitisha kauli hii kwa kutoa hoja tatu kwa kila tamthiliya kati ya tamthiliya mbili ulizosoma.